# SULIMO JULAI 2025

**MWONGOZO**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 1**

1. Umeteuliwa kuwa katibu wa jopo lililoundwa kuchunguza matatizo yanayokumba wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Andika ripoti hiyo.

**Muundo**

**1. Kichwa**

Kitaje mambo yafuatayo:

i. Neno ‘ripoti’
ii. Ripoti ni ya kina nani
iii. Inahusu nini
iv. Mahali
v. Wakati

**Tanbihi:** Kichwa kiandikwe kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari. Mwanafunzi asitie kitone.

Mfano:

**RIPOTI YA JOPO LILILOTEULIWA KUCHUNGUZA MATATIZO YANAYOKUMBA WANAFUNZI WA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA, MWAKA 2025**

**2. Utangulizi**

i. Mwanafunzi aeleze kwa kifupi kuhusu usuli wa mada.
ii. Anaweza kutaja aliyebuni jopo hilo.
iii. Aidha, mwanafunzi aeleze kipindi cha wakati walichopewa kufanya utafiti na pia kuwasilisha matokeo ya utafiti wao na kwa nani.
iv. Aorodheshe wanajopo pamoja na vyeo vyao kuanzia kwa mwenyekiti.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**3. Mbinu za ukusanyaji data**

Mwanafunzi aeleze mambo yafuatayo:

i. Maeneo waliyoteua kufanya utafiti/shule
ii. Mbinu za ukusanyaji data walizotumia.
iii. Walengwa/mbinu hizi zilitumika kwa kina nani?

**4. Matokeo ya uchunguzi/utafiti**

Mwanafunzi aeleze matokeo ya utafiti wao chini ya vijimada vidogo.

Hii ndio sehemu inayojibu swali.

Mifano ya hoja:

i. Matumizi ya dawa za kulevya
ii. Shinikizo la rika
iii. Ukosefu wa karo
iv. Adhabu kali kutoka kwa walimu
v. Migomo ya walimu
vi. Migomo ya wanafunzi
vii. Ukosefu wa usalama katika baadhi ya maeneo
viii. Uhaba wa vifaa vya kufundishia
ix. Uhaba wa walimu
x. Kuzuka kwa magonjwa ya kuambukiza shuleni kama vile kipindupindu.
xi. Mitaala mipana
xii. Kubaguliana na wanafunzi
xiii. Kutokea kwa mioto inayoteketeza shule hivyo kuathiri shughuli ya ufundishaji
xiv. Kuhamishwa kwa walimu
xv. Kuwepo kwa mitihani inayowatia wanafunzi hofu.

**Tanbihi:** ***kila tatizo liandamane na pendekezo.***

***Kadiria hoja nyinginezo***



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**5. Matatizo**

Ikiwa matatizo yapo, yaorodheshwe.

Hii sio sehemu ya lazima, hivyo mtoto asiadhibiwe ikiwa hakuandika.

**6. Hitimisho**

Mwanafunzi ahitimishe kwa kufanya muhtasari wa hoja alizotoa katika sehemu ya matokeo ya uchunguzi.

**7. Mapendekezo**

Mwanafunzi aorodheshe mapendekezo kwa nambari.

Anakili mapendekezo haya jinsi yanavyotokea katika sehemu ya matokeo ya uchunguzi.

Hatimaye sahihi, jina la mwandishi na cheo chake katika uandalizi wa ripoti huandikwa.

**Mfano wa mapendekezo**

1. Ushauri nasaha wa mara kwa mara utolewe kwa wanafunzi dhidi ya matumizi yad awa za kulevya.
2. wanafunzi wahimizwe kujiandaa vyema na mapema ili kuondoa hofu ya mitihani.
3. Serikali ishughulikie matakwa ya walimu kwa muda ufaao ili kupunguza migomo.
4. Walimu wanaowaadhibu wanafunzi wachukuliwe hatua za kisheria.
5. Serikali ihakikishe kuwa imetenga pesa za kutoka ili kununua vifaa vya kufundishia.
6. wanafunzi wanaogoma na kuchoma shule wachukuliwe hatua za kisheria.
7. Serikali iwaajiri walimu zaidi.

*KaranuJ*

Karanu Juma

Katibu wa jopo

08/09/2025



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**SWALI LA PILI**

2. Kama Mhariri wa Gazeti la Pevuka, andika tahariri ukieleza namna ya kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

**Muundo**

Jina la Gazeti na tarehe

Gazeti la Pevuka Tarehe: Julai 7, 2020

**Namna ya kuimarisha mshikamano wa kitaifa.**

**Utangulizi:** Pawe na utangulizi mwafaka.

**Mwili:** Hoja/maudhui 8 yatolewe na kujadiliwa hapa.

- Zingatia sentensi mada mwanzoni mwa kila aya.
- Ufafanuzi utolewe kwa mifano au takwimu pastahilipo.

Hitimisho:

Lisistize haja mshikamano katika taifa kwa muhtasari.

Tamati: Lionyeshe

- Jina la mhariri: Juma Mlachake
- Cheo: Mhariri
- Jina la shirika: Gazeti la Pevuka

**Namna ya kuimarisha mshikamano wa kitaifa.**

- Ugavi sawa wa rasilmali.
- Utowaji sawa wa ajira.
- Kupiga vita ufisadi.
- Kulaani ukabila.
- Kuhamasisha wanajamii kuhusu umuhimu wa mshikamano katika taifa.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

- Kuchopeka katika baadhi ya masomo shuleni na vyuoni mada zinazohusu mshikamano wa kitaifa.
- Kuwachukulia hatua kali wanaomiliki silaha hatari kinyume na sheria.
- Sheria kuzingatiwa kikamilifu zinazolinda mshikamano wa kitaifa.
- Kuruhusu tamasha na hafla mbalimbali kuadhimishwa kuhusu mshikamano wa kitaifa.
- Kuhimiza vyombo vya habari kuwa kielelezo katika kueneza mshikamano wa taifa.
- Dini na dhehebu mbalimbali kuthaminiana / kuheshimiana.
- Kusajili wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali za taifa kusomea shule moja.
- Viongozi kuhubiri kuhusu mshikamano.
- Wazazi kukuza maadili ya mshikamano kwa watoto.
- Mabango na vipeperushi viandaliwe vinavyotangaza mshikamano.

## SWALI LA TATU

3. Mwanafunzi atunge kisa kinachooana kimaana na methali hii.
   Maana ni kwamba anayejiingiza katika jambo hatari, hukumbwa na matatizo mwishowe

**Mfano:**

- Mtu kujiingiza katika ulevi na kukumbwa na matatizo kama kupofuka na vifo
- Jamii kushinikiza wasichana kukeketwa na mwisho kukumbwa na maradhi, kuvuja damu na kuaga.
- Mja kujiingiza katika vitendo viovu kama kuua watu na mwisho kupigwa risasi na kuaga
  Mwanafunzi azingatie sehemu mbili za methali. Akishughulikia upande mmoja, basi asipite alama kumi.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**SWALI LA NNE**

Msimulizi anafaa asimulie hali mpya aliyoingia baada ya kutoka kwa hali nyingine.

Hali mpya iwe inahitaji kujitolea ( ndiposa neno kukabiliana). Kuna matumaini ya hali nzuri au kuna hali nzuri (tabasamu na uchungu kuyeyuka.)

Hali ya awali haikuwa nzuri.

Masimulizi yanayoashiria yafuatayo yaweza kujitokeza.

i. Msimulizi anaweza kuendeleza kisa kwa kusimulia alivyokabiliana na hali mpya na katika masimulizi aonyeshe hali ya zamani.

ii. Msimulizi anaweza kutumia mbinu rejeshi kuonyesha hali ya awali kisha asimulie jinsi alivyokabiliana na hali mpya.

iii. Anaweza kuelezea hali ya huzuni kama vile kuhusika katika ajali na baadaye kuhitajika kufanyiwa matibabu ambayo yangehitaji akatwe kiungo kama vile mguu au mkono ili apone na aridhie na hali hiyo.

iv. Apatikane na ugonjwa ambao atahitajika kutumia dawa maishani mwake ndipo aendelee kuishi.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes